# CHIMBUKO LA REJEA ZA
# "MAFUNDISHO YA BUDDHA"

Majina kwa kifupi: DN-Dīgha Nikāya
MN-Majjhima Nikāya
SN-Saṃyutta Nikāya
AN-Aṅguttara Nikāya

## BUDDHA

| *Kifungu* | *Ukurasa* | *Mstari* | *Chimbuko* |
|---|---|---|---|
| Sura ya 1 | | | |
| 1 | 2 | 1 | Mafundisho mbali mbali |
| | 4 | 19 | AN 3-38, Sukhumālā-sutta |
| | 5 | 8 | MN 3-26, Ariyapariyesana-sutta |
| | 5 | 13 | Mafundisho mbali mbali |
| | 6 | 13 | MN 9-85, Bodhirājakumāra-sutta |
| | 6 | 17 | Mafundisho mbali mbali |
| | 7 | 5 | Sutta-nipāta 3-2, Padhāna-sutta |
| | 7 | 11 | Mafundisho mbali mbali |
| | 7 | 6 | Vinaya, Mahāvagga 1 |
| | 9 | 6 | DN 16, Mahāparinibbāna-sutta |
| 2 | 10 | 3 | DN 16, Mahāparinibbāna-sutta |
| | 10 | 16 | Parinibbāna-sutta |
| | 12 | 12 | Parinibbāna-sutta |
| | 12 | 19 | DN 16, Mahāparinibbāna-sutta |
| Sura ya 2 | | | |
| 1 | 14 | 1 | Amitāyur-dhyāna & Vimalakīr-ti-nirdeśa sūtras |
| | 14 | 5 | Śūraṃgama-sūrta |

| *Kifungu* | *Ukurasa* | *Mstari* | *Chimbuko* |
|---|---|---|---|
| | 14 | 9 | Vimalakīrti-nirdeśa & Mahāparinirvāṇa sūtras |
| | 15 | 2 | Saddahrmapuṇḍarīka-sūtra 16 |
| | 15 | 17 | Mahāyāna-jātaka-cittabhūmi-parīkṣa-sūtra |
| | 15 | 22 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| 2 | 17 | 11 | Saddahrmapuṇḍarīka-sūtra 3 |
| | 18 | 11 | Saddahrmapuṇḍarīka-sūtra 4 |
| | 18 | 22 | Saddahrmapuṇḍarīka-sūtra 5 |
| 3 | 21 | 3 | Saddahrmapuṇḍarīka-sūtra 16 |
| Sura ya 3 | | | |
| 1 | 24 | 1 | Avataṃsaka-sūtra 5 |
| | 25 | 1 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 25 | 6 | Avataṃsaka-sūtra |
| | 25 | 13 | Suvarṇaprabhāsottamarāja-sūtra 3 |
| 2 | 27 | 14 | Avataṃsaka-sūtra |
| | 27 | 19 | Avataṃsaka-sūtra 34, Gaṇḍavyūha |
| | 28 | 3 | Smaller Sukhāvatīvyūha-sūtra |
| | 28 | 6 | Avataṃsaka-sūtra |
| | 28 | 11 | SN 35-5 |
| | 28 | 15 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| 3 | 30 | 11 | MN 8-77, Mahāsakulūdayi-sutta |
| | 31 | 4 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 31 | 15 | Laṅkāvatāra-sūtra |
| | 32 | 1 | Avataṃsaka-sūtra 32 |

| *Kifungu* | *Ukurasa* | *Mstari* | *Chimbuko* |
|---|---|---|---|
| | 32 | 15 | Saddharmapuṇḍarīka-sūtra 25 |
| | 32 | 20 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 33 | 7 | Saddharmapuṇḍarīka-sūtra 2 |
| | 33 | 13 | Saddharmapuṇḍarīka-sūtra 2 |
| | | | DHARMA |
| Sura ya 1 | | | |
| 1 | 36 | 1 | Vinaya, Mahāvagga 1-6 & SN 56-11-12, Dhammacakra-pravartana-sutta |
| | 37 | 13 | Itivuttaka 103 |
| | 37 | 23 | MN 2, Sabbāsava-sutta |
| | 38 | 5 | Sūtra ya sehemu arobaini na mbili 18 |
| | 38 | 17 | Śrīmālādevīsiṃhanāda-sūtra |
| 3 | 40 | 10 | Avataṃsaka-sūtra 22, Daśa-bhūmika |
| Sura ya 2 | | | |
| 1 | 44 | 1 | MN 4-35, Cūḷasaccaka-sutta |
| | 46 | 3 | AN 5-49, Rajah-muṇḍa-sutta |
| | 46 | 13 | AN 4-185, Samaṇa-sutta |
| | 46 | 18 | AN 3-134, Uppāda-sutta |
| 2 | 47 | 1 | Laṅkāvatāra-sūtra |
| | 47 | 5 | Avataṃsaka-sūtra 2 |
| | 47 | 13 | Avataṃsaka-sūtra 16 |
| | 48 | 2 | Avataṃsaka-sūtra 22, Daśa- |

| *Kifungu* | *Ukurasa* | *Mstari* | *Chimbuko* |
| --- | --- | --- | --- |
| | | | bhūmika |
| | 48 | 13 | Laṅkāvatāra-sūtra |
| | 48 | 18 | AN 4-186, Ummagga-sutta |
| | 48 | 22 | Dhammapada 1, 2, 17, 18 |
| | 49 | 12 | SN 2-1-6, Kāmada-sutta |
| 3 | 49 | 22 | Avataṃsaka-sūtra 16 |
| | 50 | 6 | Laṅkāvatāra-sūtra |
| | 50 | 21 | MN 3-22, Alagaddūpama-sutta |
| | 51 | 17 | Laṅkāvatāra-sūtra |
| | 51 | 21 | Laṅkāvatāra-sūtra |
| 4 | 54 | 3 | Vinaya Mahāvagga 1-6 |
| | 54 | 13 | SN 35-200, Dārukkhandha-sutta |
| | 55 | 7 | Laṅkāvatāra-sūtra na nyinginezo |
| | 55 | 21 | MN 2-18, Madhupiṇḍika-sutta |
| | 56 | 9 | Laṅkāvatāra-sūtra |
| | 56 | 22 | Laṅkāvatāra-sūtra |
| | 57 | 16 | Vimalakīrti-nirdeśa-sūtra |
| | 59 | 18 | Avataṃsaka-sūtra 34, Gaṇḍavyūha |
| | 60 | 2 | Laṅkāvatāra-sūtra na nyinginezo |
| Sura ya 3 | | | |
| 1 | 61 | 1 | Vinaya Mahāvagga 1-5 |
| | 61 | 14 | Vinaya, Cūḷavagga 5-21 |
| | 62 | 1 | Śūraṃgama-sūtra |

| *Kifungu* | *Ukurasa* | *Mstari* | *Chimbuko* |
|---|---|---|---|
| 2 | 66 | 18 | Śūraṃgama-sūtra |
| | 68 | 13 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 68 | 20 | Saddharmapuṇḍarīka-sūtra 7 & Śūraṃgama-sūtra |
| | 69 | 11 | Avataṃsaka-sūtra 32 |
| | 69 | 16 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 69 | 20 | Brahmajāla-sūtra |
| | 70 | 6 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| 3 | 71 | 1 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| Sura ya 4 | | | |
| 1 | 76 | 1 | Śrīmālādevīsiṃhanāda-sūtra |
| | 77 | 7 | AN 2-11 |
| | 77 | 11 | Itivuttaka 93 |
| | 77 | 18 | Vinaya, Mahāvagga |
| | 78 | 4 | AN 3-68, Aññātiṭṭhika-sutta |
| | 78 | 18 | AN 3-34, Āḷavaka-sutta |
| | 79 | 9 | Vaipulya-sūtra |
| | 79 | 14 | Vinaya, Mahāvagga 1-6, Dhammacakrapravartana-sutta |
| | 79 | 17 | MN 2-14, Cūḷadukkhakkhandha-sutta |
| | 80 | 9 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 81 | 6 | Itivuttaka 24 |
| 2 | 83 | 3 | MN 6-51, Kandaraka-suttanta |
| | 83 | 16 | AN 3-130 |
| | 83 | 22 | AN 3-113 |

| *Kifungu* | *Ukurasa* | *Mstari* | *Chimbuko* |
|---|---|---|---|
| 3 | 84 | 12 | Itivuttaka 100 |
| | 85 | 1 | Saṃyuktaratnapiṭaka-sūtra |
| | 85 | 20 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 87 | 4 | AN 3-62 |
| | 87 | 17 | AN 3-35, Devadūta-sutta |
| | 88 | 23 | Therīgāthā Aṭṭhakathā |
| 4 | 89 | 1 | Sukhāvatīvyūha-sūtra vol. 2 |
| Sura ya 5 | | | |
| 1 | 96 | 1 | Sukhāvatīvyūha-sūtra vol. 1 |
| | 99 | 8 | Sukhāvatīvyūha-sūtra vol. 2 |
| | 100 | 16 | Amitāyur-dhyāna-sūtra |
| 2 | 104 | 1 | Sukhāvatīvyūha-sūtra ndogo |

## NJIA YA MATENDO

| | | | |
|---|---|---|---|
| Sura ya 1 | | | |
| 1 | 108 | 1 | MN 2, Sabbāsava-sutta |
| | 109 | 21 | MN 3-26, Ariyapariyesana-sutta |
| | 110 | 10 | SN 35-206, Chapāna-sutta |
| | 111 | 6 | Sūtra ya sehemu arobaini na mbili 41-2 |
| | 113 | 13 | MN 2-19, Dvedhāvitakka-sutta |
| | 114 | 4 | Dhammapada Aṭṭhakathā |
| 2 | 115 | 3 | AN 3-117 |
| | 115 | 15 | MN 3-21, Kakacūpama-sutta |
| | 118 | 15 | MN 3-23, Vammīka-sutta |

| *Kifungu* | *Ukurasa* | *Mstari* | *Chimbuko* |
|---|---|---|---|
| | 120 | 4 | Jātaka IV-497, Mātaṅga-Jātaka |
| | 123 | 13 | Sūtra ya sehemu arobaini na mbili 9 |
| | 123 | 21 | Sūtra ya sehemu arobaini na mbili 11 |
| | 124 | 12 | Sūtra ya sehemu arobaini na mbili 13 |
| | 125 | 8 | AN 2-4, Samacitta-sutta |
| 3 | 126 | 1 | Saṃyuktaratnapiṭaka-sūtra |
| | 134 | 16 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 135 | 9 | Saṃyuktaratnapiṭaka-sūtra |
| Sura ya 2 | | | |
| 1 | 139 | 1 | MN 7-63, Cūḷamālunkya-suttanta |
| | 140 | 23 | MN 3-29, Mahāsāropama-sutta |
| | 142 | 7 | Mahāmāyā-sūtra |
| | 142 | 19 | Theragāthā Aṭṭhakathā |
| | 144 | 6 | MN 3-28, Mahāhatthipadopama-sutta |
| | 144 | 19 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 145 | 6 | Avadānasátaka-sūtra |
| | 146 | 6 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 147 | 18 | Pañcaviṃśati-sāhasrikā-prajñāpāramitā-sūtra |
| | 149 | 1 | Avataṃsaka-sūtra 34, Gaṇḍa- |

| *Kifungu* | *Ukurasa* | *Mstari* | *Chimbuko* |
|---|---|---|---|
| | | | vyūha |
| 2 | 150 | 14 | AN 3-88 |
| | 151 | 10 | AN 3-81 |
| | 151 | 16 | AN 3-82 |
| | 152 | 7 | Parinibbāna-sutta vol. 2 |
| | 153 | 5 | MN 14-141, Saccavibhanga-sutta |
| | 154 | 7 | Parinibbāna-sutta vol. 2 |
| | 154 | 19 | AN 5-16, Bala-sutta |
| | 155 | 1 | Avataṃsaka-sūtra 6 |
| | 155 | 16 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 156 | 4 | Ṣaṃyuktaratnapitaka-sūtra |
| | 156 | 17 | Suvarṇaprabhāsa-sūtra 26 |
| | 157 | 5 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 158 | 2 | Theragāthā Aṭṭhakathā |
| | 158 | 17 | Jātaka 55, Pañcāvudha-Jātaka |
| | 159 | 20 | Itivuttaka 39 & 40 |
| | 160 | 6 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 160 | 9 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 160 | 11 | AN 5-12 |
| | 160 | 16 | Parinibbāna-sutta |
| | 161 | 1 | Śūraṃgama-sūtra |
| 3 | 162 | 3 | SN 55-21 & 22, Mahānāma-sutta |
| | 162 | 17 | AN 5-32, Cundī-sutta |
| | 163 | 5 | Vimalakīrti-nirdeśa-sūtra |

| *Kifungu* | *Ukurasa* | *Mstari* | *Chimbuko* |
|---|---|---|---|
| | 163 | 16 | Śūraṃgama-sūtra |
| | 163 | 22 | Sukhāvatīvyūha-sūtra vol. 2 |
| | 164 | 8 | SN 1-4-6 |
| | 164 | 11 | Avataṃsaka-sūtra 33 |
| | 165 | 5 | Avataṃsaka-sūtra 24 |
| | 165 | 16 | Suvarṇaprabhāsa-sūtra 4 |
| | 166 | 1 | Amitāyur-dhyāna-sūtra |
| | 166 | 4 | Sukhāvatīvyūha-sūtra |
| | 166 | 9 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 167 | 5 | MN 2-16, Cetokhila-sutta |
| | 167 | 20 | Sukhāvatīvyūha-sūtra vol. 2 |
| 4 | 168 | 12 | Dhammapada |
| | 176 | 1 | SN 1-6-59 |
| | 176 | 14 | AN |
| | 176 | 19 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |

UNDUGU

Sura ya 1

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | 178 | 1 | Itivuttaka 100 & MN 1-3, Dhammadāyāda-sutta |
| | 178 | 7 | Itivuttaka 92 |
| | 178 | 16 | Vinaya, Mahāvagga 1-30 |
| | 178 | 16 | MN 4-39, Mahā-assapura-sutta |
| | 180 | 19 | MN 4-40, Cūḷa-assapura-sutta |
| | 181 | 16 | Saddharmapuṇḍarīka-sūtra 10 |
| | 181 | 21 | Saddharmapuṇḍarīka-sūtra 10 |

| *Kifungu* | *Ukurasa* | *Mstari* | *Chimbuko* |
|---|---|---|---|
| | 182 | 7 | Saddharmapuṇḍarīka-sūtra 14 |
| 2 | 183 | 15 | SN 55-37, Mahānāma-sutta |
| | 184 | 3 | AN 3-75 |
| | 184 | 9 | SN 55-37, Mahānāma-sutta |
| | 184 | 14 | SN 55-54, Gilāyanaṃ-sutta |
| | 184 | 20 | Avataṃsaka-sūtra 22 |
| | 186 | 6 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 188 | 20 | Avataṃsaka-sūtra 7 |
| | 191 | 10 | Mahāmāyā-sūtra |
| | 192 | 8 | Avataṃsaka-sūtra 21 |
| | 193 | 2 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| Sura ya 2 | | | |
| 1 | 194 | 1 | DN 31, Siṅgālovāda-sutta |
| | 199 | 1 | AN 2-4, Samacitta-sutta |
| | 199 | 17 | AN 3-31 |
| | 200 | 1 | Jātaka 417, Kaccāni-Jātaka |
| | 201 | 15 | DN 31, Siṅgālovāda-sutta |
| | 202 | 1 | Dhammapada Aṭṭhakathā 1 |
| 2 | 203 | 6 | AN 4-197 |
| | 204 | 3 | AN 5-333 Uggaha-sutta |
| | 204 | 19 | (Maoni ya Wa-Burma) |
| | 205 | 11 | AN 7-59, Sujāta-sutta |
| | 207 | 4 | DN 16, Mahāparinibbāna-sutta |
| 3 | 208 | 8 | Śrīmālādevīsiṃhanāda-sūtra |
| | 210 | 9 | DN 16, Mahāparinibbāna-sutta |
| | 211 | 10 | Avataṃsaka-sūtra 34, Gaṇḍav- |

| *Kifungu* | *Ukurasa* | *Mstari* | *Chimbuko* |
|---|---|---|---|
| | | | yūha |
| | 212 | 17 | Suvarṇaprabhāsa-sūtra 12 |
| | 213 | 15 | Bodhisattva-gocaropāya-viṣa-yavikurvana-nirdeśa-sūtra |
| Sura ya 3 | | | |
| 1 | 220 | 1 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 221 | 13 | AN 3-118, Soceyyan-sutta |
| | 223 | 5 | SN |
| | 223 | 15 | Vinaya, Mahāvagga 10-1 & 2 |
| | 224 | 1 | DN 16, Mahāparinibbāna-sutta |
| | 225 | 6 | Vinaya, Mahāvagga 10-1 & 2 |
| 2 | 227 | 16 | SN |
| | 228 | 13 | Antarābhava-sūtra |
| | 228 | 19 | Vimalakīrti-nirdeśa-sūtra |
| | 229 | 22 | Mahāparinirvāṇa-sūtra |
| | 230 | 17 | Sukhāvatīvyūha-sūtra ndogo |
| | 231 | 1 | Sukhāvatīvyūha-sūtra |
| | 231 | 14 | Vimalakīrti-nirdeśa-sūtra |
| 3 | 232 | 1 | Dhammapada Aṭṭhakathā 1 |
| | 232 | 14 | AN 34-2 |
| | 233 | 8 | Dhammapada Aṭṭhakathā 1 |
| | 234 | 1 | AN 5-1 |
| | 234 | 5 | Sarvāstivāda-saṃghavedaka-vastu 10 |
| | 234 | 19 | MN 9-86, Aṅgulimāla-sutta |
| | 235 | 18 | AN 26 |

# VIAMBATISHO

# HISTORIA FUPI YA UBUDDHA

## 1. INDIA

Mojawapo ya matukio maalum ya kukumbukwa, katika historia ya kiroho ya binadamu lilijitambulisha wakati "mwanga wa Asia" ulipoangaza katika sehemu ya kati ya India, au kwa maneno mengine chemchem ya Hekima Kuu na Huruma ilipobubujika kule, ambayo imetokea kustawisha moyo wa binadamu kwa muda wa karne nyingi hadi sasa.

Buddha Gautama, aliyekuja kujulikana kwa wafuasi wa baadaye kama Shakyamuni au " Mtu wa Hekima katika ukoo wa Shakya" aliacha mji wake akawa mwombaji na akafunga safari kuelekea kusini hadi magadha. Inakisiwa na kuaminiwa kuwa Buddha aliupata Uongofu (Nuru) katikati ya karne ya tano KK chini ya mti uitwao Bodhi. Kuanzia hapo aliendelea na juhudi zake bila kuchoka kwa muda wa miaka 45 akihubiri mafundisho ya hekima, na Huruma hadi alipokutana na " Kifo chake kikuu" ambapo aliingia Maha - pari- Nirvana, wakati wote akiwa anafundisha juu ya hekima na huruma. Matokeo yake, Mabuddha waliendelea kujitokeza katika falme na makabila mbalimbali katikati ya India.

Mnamo nyakati za utawala wa Mfalme Asoka (aliyetawala: 268 - 232 K.K) mtawala wa tatu wa ufalme wa Maurya, mafundisho ya Buddha Gautama yalienea katika nchi yote ya India na hata nje ya mipaka yake.

Maurya ilikuwa ya kwanza katika muungano wa falme za India. Wakati wa mtawala wake wa kwanza, Chandragupta (alitawala : 316 - 293 K.K au nyakati kama hizo) ufalme huu ulikuwa ukitawala milki kubwa kuanzia milima ya Himalaya Kasakazini hadi katika Ghuba ya Bengal Mashariki, kutoka katika milima ya Hindu Kush Magharibi na ng'ambo ya milima ya Vindhya sehemu ya Kusini.

Mfalme Asoka aliendelea kuipanua milki hii hadi nyanda za Deccan alipoiteka Kalinga na Sehemu nyinginezo.

Mfalme huyu anasemekana kuwa alikuwa na tabia ya gadhabu, watu wakimwita Chandāsoka (Harara Asoka). Lakini tabia yake ilibadilika aliposhuhudia maafa mabaya yaliyotokana na vita vya kuiteka Kalinga. Alipindukia kuwa mfuasi mzuri wa mafundisho ya Hekima na Huruma. Baada ya hapo, alitenda mambo mengi kama muumini wa Buddha, kati yake kazi mbili zifuatazo ni za kukumbukwa.

Kwanza, zilikuwa ni " sheria za Asoka," au dhana za utawala zilizojengwa juu ya mafundisho ya Buddha zilizochorwa juu ya nguzo za mawe, alizoamrisha zichorwe katika sehemu nyingine mbalimbali ili kueneza mafundisho ya Buddha. Pili, alituma wajumbe nje ya milki yake katika nchi mbalimbali wakieneza mafundisho ya Hekima na Huruma pande zote. Jambo la kukumbukwa ni kwamba baadhi ya wajumbe walitumwa sehemu za Syria, Misri, Krene, Makedonia na Epeiro kueneza UBuddha kwa marefu na mapana Magharibi ya dunia. Waama, Mahendra (Mahindo katika lugha ya Pāli) mjumbe aliyepelekwa Tāmraparni au Siloni (Ceylon) alifanikiwa katika " Kuanzisha mafundisho mema juu ya Lankādvīpa (Pāli, Lankādīpa) njema" na hivyo akaweka msingi wa mahali pa kuanzia kueneza mafundisho ya Buddha kwa mafanikio kisiwani.

## 2. KUSTAWI NAKUENEA KWA U - BUDDHA WA MAHAYANA

" Mkondo wa Mashariki na U - Buddha" umezungumziwa sana na wafuasi wa Buddha wa siku za kale. Lakini mnamo karne za kabla ya Kristo, sura ya U - Buddha ilielekezwa Magharibi. Ilikuwa wakati wa mwanzo wa muhula wa ukristo "sura" Ya U - Buddha ilipoanza kuelekezwa Mashariki. Walakini kabla ya kurejea kwenye jambo hili, tuzungumzie mageuzi yaliyotokea katika U - Buddha. Badiliko hili lilikuwa si jingine bali "Wimbi jipya" Inavyojulikana kama U - Buddha

wa Mahayana au Gari Kuu la U - Buddha, ambao ulikuwa unajiimarisha barabara na kujitokeza wazi katika mafundisho ya wakati huo.

Nani, lini na vipi "Wimbi jipya" lilianzishwa? Hadi sasa hakuna mwenye uwezo wa kujibu kwa usahihi maswali haya. Tunachokifahamu ni: Kwanza, mkondo ulioibuka utakuwa katika kiti kinachoitwa kizazi - fikirika sehemu ya mchanganyiko wa shule ya Mahāsaṁghika kwa makasisi waliofanikiwa wa wakati huo; Pili, ukweli ni kwamba yalikwisha kuwepo baadhi ya maelezo ya msingi ya maandiko matakatifu ya Mahayana kuanzia karne ya kwanza au ya pili BK hadi karne ya kwanza ya muhula wa ukristo. Hata wakati wazo zuri la Nāgārjuna likiungwa mkono na maandishi ya Mahayana, lilikuzwa, uwaziwazi u-Buddha wa Mahayanaa, ulizidi kujitokeza mbele katika jukwaa la historia ya dini.

Kazi iliyotendwa na U - Buddha wa Mahayana ilikuwa kubwa sana katika historia ndefu ya U - Buddha. Sasa, kwa Uchina na Japan, U - Buddha kwa nchi hizi kwa karibu historia yake yote, umestawi kwenye msingi wa Mafundisho ya Mahayana. Hili halielekei kuwa jambo geni kwani kulishakuwepo na wazo adilifu kwa wokovu wa umma, likioanisha watakatifu hai katika mtizamo wa Bodhisattvas kueneza wazo hili; zaidi ya hapo, katika kuwaunga mkono, matokeo ya kielimu katika uwanja wa elimu au saikolojia yaliyokuwa yameletwa na wanagenzi wa Mahayana yalikuwa ya maana. Katika hali hii ingawa ilihusishwa na mafundisho ya Buddha Gautama kwa upande mmoja awamu mpya za hekima na maadili ziliongezewa. Kwa nyongeza hizi mpya U - Buddha ulipata nguvu na harufu mpya zilizoboresha nchi za Mashariki kama kasi ya mkondo wa mto mkubwa.

## 3. MASHARIKI YA KATI

China ilipata habari za U - Buddha kutoka katika nchi za Asia ya kati. Hivyo basi tunapozungumzia mafundisho kuenea kutoka India hadi

Uchina, hatuna budi kuzungumzia Barabara ya Hariri. Barabara hii ikipitia katika nchi zisizo na mipaka katikati ya Asia kuunganisha Magharibi na Mashariki, na ilikuwa katika umri wa Mfalme Wu wa Nasaba ya Han ( aliyetawala 140 - 87 K.K), njia hii ilipofunguliwa. Wakati huo milki ya Han ilienea hadi Magharibi na katika nchi zilizoipakana kama Ferghana, Sogdiana, Tukhara, na hata Parthia, na moyo wa kibiashara uliokuwa umeingizwa na Alexander mkuu ulikuwa bado unapamba moto. Katika njia hii iliyopita katika nchi hizo, hariri ilichukua nafasi muhimu sana na ndiyo sababu ikaitwa Barabara ya Hariri. Kuanzia labda muda kidogo kabla au baada ya muda wa mwanzo wa muhula wa ukristo India na Uchina zilianza uhusiano wa kiutamaduni kwanza kwa njia ya barabara ya biashara. Kwa hiyo barabara inaweza kusemwa kuwa imekuwa njia ya U - Buddha vilevile.

## 4. UCHINA

Historia ya U - Buddha wa Kichina inaanza na wao kukubali maandiko ya Buddha na tafsiri yake iliyofuata. Maandiko ya zamani sana yasemekana kuwa ni "Ssu - Shih - êr - châng - ching"
(Sutra katika sehemu arobaini na mbili zilizotamkwa na Buddha)". Tafsiri iliyofanywa na Kāśyapamātaṅga na wengine wakati wa kipindi cha Ying - P'ing (58 - 76 B.K) cha Mfalme King Ming wa milki iliyofuatia ya Han ya Mashariki ingawa sasa inadhaniwa kuwa hadithi hiyo siyo ya kweli. Mtizamo wa pamoja sasa unatoa shukrani kwa An - shih - kao aliyeshughulika katika kutafsiri huko Lo - yang kuanzia mwaka 148 hadi 171 B.K. Kuanzia sasa hadi wakati wa Nasaba ya Kaskazini ya Sung (960 - 1129 B.K) kazi ya kutafsiri iliendelea kwa zaidi ya miaka elfu moja.

Mnamo miaka ya mwanzo watu waliofanya kazi za Uhasisi maandiko na kufanya tafsiri zake wengi wao walikuwa makasisi kutoka nchi za katikati ya Asia. Kwa mfano An - shih - kao, aliyetajwa hapo juu, alitoka Parthia, K'ang - sêng - k'ai, kutoka eneo la Samarkand alikwenda Lo - yang mnamo karne ya tatu na akatafsiri

"Sukhāvativyūha" (Kitabu cha maisha yasiyo na kikomo). Aidha, Chu - fa - hu au Dharmaraksha, anayejulikana kama mfasiri wa "Saddharma - puṇḍarīka" alitoka Tukhāra na aliishi Lo - yang tangu mwisho wa karne ya tatu hadi sehemu ya mwanzo ya karne ya nne. Wakati alipojitokeza kumārajīva, kutoka Kucha, mnamo mwanzoni mwa karne ya tano, kazi ya kutafsiri ilikuwa imefikia kiwango cha juu sana  huko Uchina.

Kuanzia wakati huo, makasisi kutoka Uchina walianza kuitembelea India kujifunza Sanskrit. Mtangulizi wa makasisi hao alikuwa Bwana Fa-hsien (339-420? BK). Aliondoka Ch'ang-an mnamo 399 kwenda India na alirudi nyumbani baada ya miaka kumi na mitano. Kasisi mteule kati ya wale walioitembalea India alikuwa Hsuan - chuang (600-664 BK)  aliyefika huko mwaka 627 na kurudi nyumbani katika mwaka 645 baada ya miaka kumi na tisa. Tena I - ching (635 - 713 B.K) (bila ya kumchanganya na jina la kitabu I - ching) alifunga safari kwenda India kwa njia ya bahari mnamo 671 na alirudi nyumbani kwa njia hiyo hiyo baada ya miaka ishirini na mitano

Makasisi hawa waliitembelea India wao wenyewe kujifunza Sanskrit na kurudi nyumbani na maandiko waliyokuwa wameyachagua, wakiwa watangulizi katika kazi za kutafsiri. Uwezo wa kiisimu wa Lugha aliokuwa nao Hsuan - chuang ulikuwa wa hali ya juu na kwa juhudi zake, kazi ya kutafsiri maandiko ilikuwa imepiga hatua kubwa. Kazi za awali zilizofanywa na watangulizi kama vile Kumārajīva inaitwa "Tafsiri za kale" na kazi za Hsuan - chuanga na wafasiri waliofuata zinaitwa "Tafsiri mpya" na wanagenzi wa U-Buddha katika nyakati zilizofuatia.

Kutokana na wingi wa juzuu walizokuwa wamezitafsiri kutoka Sanskrit mwelekeo wa fikra na shughuli za kidini za wanazuoni hawa, taratibu, ingawa kwa nguvu ziligeukia katika shari. Ilijitokeza dhahiri hali ya ujamii na tabia halisi ya mahitaji na kujiamini. Ukweli kwamba makasisi katika hatua za mwanzo walielekeza mioyo yao kwenye imani ya msingi wa "Hakuna kinachodumu" hasa inayozungumziwa katika Prajñā ya Sutra ilikuwa ni udhihirisho wa mwelekeo huu. Baadaye

walitupilia mbali kile kilichoitwa "Hinayana", au Gari kuu. Waama mwelekeo huu taratibu ulijitokeza katika dhehebu la Tendai na inasemekana kuwa ulikuwa umefikia kilele chake lilipojitokeza dhehebu la Zen.

Ilikuwa katika sehemu ya pili ya karne ya Sita wakati Dhehebu la Tendai liliposhuhudia ukamilifu wake katika Uchina, iliyokamilishwa na Tendai Daishi, Chih - i (538 - 597 B.K) mzee wao mkuu wa tatu. Alikuwa mmojawapo wa watu mashuhuri sana katika imani ya U-Buddha na uchambuzi wa makini katika mafundisho ya Buddha katika Vipindi vitano na kanuni nane alizozitengeneza mtakatifu huyu yamekuwa na mvuto mkubwa katika U - Buddha wa China pamoja na Japan.

Uchambuzi utaonyesha kuwa katika Uchina, Sutras nyingi zililetwa Uchina bila kujua wala kujali mpangilio wa asili au chimbuko lake na Sutras hizo zilitafsiriwa kama zilivyopokelewa. Katika mlundikano wa Sutras hizi lilijitokeza tatizo la kuelewa asili na tathimini zao. Ilikuwa muhimu kuupokea U - Buddha kwa ujumla na kuonyesha jinsi mtu atakavyosimama kufuatana na uelewa wake. Katika tathmini ya Sutras, muelekeo wa mtizamo wa Kichina, kwanza ni kwa watangulizi. Juu ya yote, ile ya Chih - i ilikuwa imepangwa kimantiki na hivyo rahisi kusadikika. Lakini baada ya kazi za uchambuzi wa U - Buddha wa kisasa kujitokeza, kazi yake Chih - i ilipoteza umaarufu wake.

Ndani ya historia ya U-Buddha katika Uchina "Lilokuwa la Mwisho" ilikuwa Dhehebu la Zen. Mwanzilishi wake inasemekana kuwa ni Śramana, kutoka nchi ya ugenini, au Bodhidharma (-528 B.K); lakini, mbegu aliyoipanda ilichanua maua baada ya Hui - nêng (638 - 713 B.K) mzee wa sita katika historia hii. Baada ya karne ya nane dhehebu hili katika Uchina lilishatoa makasisi wengi wenye vipaji wakifuatana huku ustawi wa Zen ukidumishwa kwa muda wa karne nyingi.

Inaonekana wazi kuwa kulikuwa na fikra mpya katika U - Buddha, iliyoweza kuzama katika asili ya Wachina. Haikuwa kitu kingine ila U

- Buddha uliopambwa na mtizano wa fikra wa kichina. Na kumbe mtiririko wa mafundisho ya Buddha Gautama pamoja na wimbi hili jipya lililoongezeka, yalifanya mto upanuke na ukatokea kurutubisha nchi zote za Mashariki.

## 5. JAPAN

Historia ya U - Buddha katika Japan ilianza katika karne ya sita. Mnamo mwaka 538 B.K, Mfalme wa Paikche (au Kudara, Korea) alituma ujumbe wake kuwasilisha sura ya U - Buddha na vitabu vya Sutras kwenye Baraza Tukufu la Mfalme Mkuu Kinmei. Huu ulikuwa mwanzo wa U - Buddha katika nchi hii. Kwa hiyo historia ya dini katika Japan ina umri wa zaidi ya miaka 1,400 sasa.

Katika historia hii ndefu tunaweza kufikiria U - Buddha wa Japan kwa kuihusisha na mitizamo mitatu. Wa kwanza unaweza kuwekwa kwenye U - Buddha wa mnamo karne ya saba, na nane. Kuonyesha hii kwa wazi ni ushahidi wa Hekalu la Horyuji (607 B.K) na Hekalu la Todaiji ( 752 B.K) yaliyojengwa wakati huo. Tukichunguza wakati huu kuna ukweli ambao hauwezi kusahaulika kuwa mkondo wa utamaduni ulikuja juu kuliko kawaida katika Asia yote, na ustaarabu wa Magharibi ulitupwa gizani. Msukumo imara na wa ajabu ulianza kujengeka kwa nguvu katika Asia. Katika Uchina, Mashariki ya katikati, India na nchi za Bahari ya Kusini, Shughuli za izidathira, kidini na kisanaa ziliendelea kwa nguvu. Kuunganisha misukumo hii U - Buddha ulikuwa ukitakasa nchi za Mashariki kwa mkondo wake mkuu wa huruma na utu. Na msukumo huu mpya wa utamaduni wa Kijapani kama unavyodhihirishwa na ujenzi wa mahekalu mazuri ya Horyuji na Todaiji, na pia kazi nzuri za kidini na kisanaa zilizojitokeza kwa kuhusiana na utamaduni ulivyoingia ndani hadi kingo za ncha ya Mashariki ambao ulikuwa unaikumba sehemu kubwa ya Asia.

Watu wa nchi hii, ambayo haikuwa na ustaarabu kwa miaka mingi, sasa waliogelea katika wimbi la utamaduni mkubwa; na ua la ustaarabu

lilichanua ghafla. Hii ilikuwa bahati iliyozungukia Ujapani katika karne hizo. Na mshindi mkuu mhusika wa kukua kwa utamaduni huu ni u - Buddha, mahekalu ya u - Buddha ya wakati ule yalikuwa vituo mashuhuri vya jamii, na makuhani walikuwa viongozi wa elimu mpya. Kuliinukia utamaduni mkubwa na usiokuwa wa kidini tu. Hii ilikuwa hali halisi ya u - Buddha ulioanziswa kwa mara ya kwanza katika nchi hii.

Katika karne ya tisa, makuhani wawili, Saicho (Dengyo Daishi 767 - 822) na Kukai (Kobo Daishi 774 - 835) walijitokeza na kuanzisha madhehebu mawili ambayo kwa pamoja yanaitwa u - Buddha wa Heia. Huku kulikuwa kuanziswa kwa u - Buddha wa Kijapani hasa. Walipokea u - Buddha katika msimamo na ufuasi wake halisi na wakawa watawa kuanzisha makazi ya kati ya watawa katika Milima ya Hiei na Koya. Katika muda wa miaka mitatu baada ya kuanzishwa, hadi kipindi cha Kamakura, madhehebu haya mawili Tendai na Shingon, yalikuwa na mahusiano, na yalistawi vizuri katikati ya watawala na katika viwanja na nyumba za kifalme.

Tunaweza kuupata mtizamo wa pili kwa kuangalia U-Buddha wa karne ya kumi na mbili na kumi na tatu. Walijitokeza makuhani wakuu kama Honen (1133 - 1212 B.K), Shinran (1173 - 1262 B.K) Dogen (1200 - 1253 B.K.) na Nichiren (1222 - 1282 B.K). Tunapozungunzia u - Buddha wa Japani hatuwezi kusita kutaja majina ya makuhani hawa watatu. Je, ni kwa nini karne hizo zilizotajwa zikawa na watu mashuhuri? Ni kwa sababu walikuwa wanakabiliwa na tatizo linalofanana kwa nyakati zile. Je walikabiliwa na tatizo gani? Huenda ilikuwa ni kukubalika kwa u - Buddha lakini katika njia ya pekee ya Kijapani.

Hii inaweza kutuleta kwenye swali, " Kwa nini haikuwa kweli kwamba u - Buddha ulikwishaingizwa katika nchi hii zamani kabla ya wakati huu? Ndivyo ilivyo kihistoria. Lakini ni kweli pia kuwa mamia ya miaka ilihitajika ili watu wa nchi hii waichambue na kuiumba vyakutosha dini ya kigeni ili kuifanya mali yao.

Kwa kifupi ilikuwa katika karne ya saba na nane wakati juhudi za kuukubali u - Buddha zilipoanza katika nchi hii, na matokeo yake dini ilichanua kwa nguvu kutokana na Mabuddha wa karne ya kumi na mbili na kumi na tatu.

Baada ya hapa, u - Buddha katika Ujapani iliyosimama juu ya msingi uliojengwa na makuhani maarufu, umezilinda kazi zake hadi leo. Tangu wakati ule walipojitokeza wateule, hakuna un'gavu wowote wa karne hizo umeishajitokeza tena katika historia ya u - Buddha nchini Ujapani. Hata hivyo, inaelekea kwa mwandishi wa leo kuwa kuna kitu kingine kinachotuvutia, nacho ni matunda ya uchunguzi wa kisasa katika u - Buddha wa asili.

Tangu kukubalika kwake kwa mara ya kwamza, kwa kweli u - Buddha wote katika Japani ulikuwa Mahayana, kwa mvuto na ushawishi wa u - Buddha wa kichina. Hasa baada ya kujitokeza kwa walimu mashuhuri katika karne za kumi na mbili na kumi na tatu, mafundisho ya Mahayana yalijenga wimbi kubwa na waasisi wa madhehebu wakiwa kitovu chake; Mtizamo huo unadumu hadi leo hii.
Katika historia ya u - Buddha katika Japani, uchambuzi wa uchunguzi juu ya u - Buddha wa asili ulianza baada ya kipindi cha kati cha Meiji. Sura ya Buddha Gautama ilijitokeza barabara kwa wale wote waliokuwa wanaelekea kusahau kuwa kulikuwa na Muasisi wa u - Buddha mbali na waanzilishi wa madhehebu, na pia ilidhihirishwa kwa wale ambao hawakukubali lolote lile mbali na mafundisho ya Mahayana, kwamba kulikuwa na taratibu za imani za u- Buddha. Hatua hizi mpya bado zipo katika uwanja wa wasomi na bado hazina nguvu kuamsha shauku ya kidini kwa umma. Lakini inaonekana maarifa ya watu wa nchi hii juu ya u - Buddha yanaelekea kupinda. Mwandishi angependelea kudhihirisha hatua hii na kuiita ya tatu au ya mwisho kati ya mitizamo mitatu iliyozungumziwa hapo juu.

## KUENEZWA KWA MAFUNDISHO YA BUDDHA

U-Buddha ni dini iliyojengwa juu ya mafundisho ya Shakyamuni aliyokuwa ameyafundisha kwa muda wa miaka arobaini na tano ya maisha yake. Kwa hiyo maneno aliyoyatumia katika mafundisho yake ni madhubuti na sahihi katika dini hii, na ingawa kuna milango 84,000 ya dharma na shule nyingi vyote vinatokana na maandiko ya Shakyamuni. Vitabu vile yalimoandikwa mafundisho ya Buddha vinaitwa Issaikyo au Daizokyo, maana yake mkusanyo kamili wa maandiko matakatifu.

Shakyamuni alidai usawa wa binadamu kwa bidii sana na alifundisha kwa lugha nyepesi ili kila mmoja aweze kumwelewa kwa urahisi. Aliendelea kuhubiri kwa manufaa ya watu wengi hadi dakika ya mwisho alipokufa akiwa na umri wa miaka themanini.

Baada ya kifo cha Shakyamuni, wanafunzi wake walihubiri habari ya kweli kama walivyokuwa wamesikia. Hata hivyo, kadri mafundisho yalivyoenezwa na kusimuliwa ndivyo baadhi ya tofauti zilivyojitokeza kutokana na makosa yasiyo kusudiwa yaliyotokana na hali ya wafuasi katika yale waliyodhani kuwa wameyasikia au kuyaelewa. Na kumbe, maneno ya Shakyamuni yanapaswa kuenezwa kwa usahihi na watu wote bila ubaguzi. Kwa hiyo, wengi wa makuhani wakuu walikaa pamoja kwa nia ya kurekebisha, kuunganisha na kuimarisha maneno na mafundisho wakieleza kila mmoja alichofikiri alikuwa amekisia na kwa njia hiyo wakakaa miezi na miezi wakibadilishana mawazo. Kazi iliyotokana na mkusanyiko huo inajulikana kama Ketsuju au Mafungamano. Hii inaonyesha jinsi walivyojaribu kwa uchaji wao kueneza maneno yale yale yaliyokuwa yamezungumziwa na mwalimu mkuu.

Mafundisho yalipokwisharekebishwa yaliandikwa. Kwenye maandiko yaliyoandikwa ziliongezwa tafsiri na fafanuzi na makuhani wasomi wa miaka iliyofuata na wakaiita Ron au fafanuzi. Mafundisho

ya Buddha mwenyewe, fafanuzi zilizoongezwa baadaye, na maagizo ya Buddha, yote yalikuja kuitwa Sanzokyo (Sehemu tatu za maandiko ya Buddha) au Tripitaka katika Sanskrit.

Sanzokyo au Tripitaka ina Kyozo, Ritsuzo na Ronzo; neno Zo yamaanisha chombo au mfuko. Kyo ina maana ya maandiko ya u - Buddha, Ritsu yamaanisha maagizo ya undugu ya Buddha, na Ron ni fafanuzi zilizoandikwa na makuhani wakuu.

Kulingana na desturi, u - Buddha unasemekana kuwa uliingizwa Uchina mnamo mwaka 67 B.K wakati wa utawala wa mfalme Ming katika miongozo ya mwisho ya Nasaba ya Mashariki ya Han (25 - 220 B.K). Lakini kwa uhakika ilikuwa miaka themanini na minne baadaye maandiko ya u - Buddha yalipoingizwa ndani ya Uchina na kutafsiriwa (mwaka 151 B.K) na Mfalme Huan wa nasaba ile ile. Kwa muda wa miaka 1700 kuanzia hapo juhudi za kutafsiriwa kwa maandiko katika kichina ziliendelea. Idadi ya vitabu na juzuu vilivyotafsiriwa vilifikia maandiko 1440 na juzuu 5586. Juhudi za kuhifadhi maandiko yaliyotafsiriwa ulianza mapema katika nasaba ya Wei,ila ilikuwa mnamo Nasaba ya Kaskazini ya Sung upigaji chapa wake ulipoanza. Lakini kuanzia wakati huo kazi za makuhani wakuu wa Kichina zilianza kuongezwa kwenye maandiko ya Buddha na haikuwa tena sahihi kuviita Tripitaka vitabu hivi. Ilipotawala Nasaba ya Suei vilipewa jina la Issaikyo au mkusanyo wa maandiko yote matakatifu, na ilipotawala Nasaba ya Tang viliitwa kwa jina jipya la Daizokyo au makusanyo ya maandiko yote ya u - Buddha, sheria na nyaraka.

U - Buddha uliingia Tibeti mnamo karne ya saba B.K, na muda kama miaka 150 katika karne ya tisa hadi kumi na moja B.K; juhudi ya kuyatafsiri maandiko ya Buddha iliendelea, na hakika maandiko yote yalitafsiriwa kwa wakati huo.

Kutokana na ukweli kwamba maandiko yalikuwa yametafsiriwa siyo tu katika Kikorea, Kijapani, Kisiloni, Kikambodia, Kituruki na Kiarabu, lugha zote za Mashariki na hata katika lugha za Kilatini, Kifaransa,

Kiingereza, Kijerumani na Kiitalia, tunaweza kusema kwa usahihi kuwa baraka za mafundisho ya Buddha sasa yameenea ulimwengu mzima.

Ila katika fikra nyingine, tukitafakari kuanzia kwenye aina ya tafsiri na historia ya mwanzo na chimbuko la kuenea na kustawi kwa dini hii muda wa miaka elfu mbili, kukiwa na tafsiri za vitabu zaidi elfu kumi na mbili inakuwa vigumu kupata maneno halisi na kweli yaliyozungumzwa na Shakyamuni hata kama tutatumia msaada wa Daizokyo." Kwa hiyo ni lazima kutafuta maelezo makuu kutoka " Daizokyo" na yawe msingi ambapo mtu anaweza kusimamia katika imani yake ya kidini.

Katika u - Buddha, mamlaka ya juu yamo katika maneno aliyoyasema Shakyamuni. Hivyo basi mafundisho ya u - Buddha hayana budi kuwa ni mafundisho yanayoendana na hali halisi ya maisha ya kila siku; vinginevyo yatashindwa kuamsha moyo wa mtu kutoka katika kilindi chake kuelekea kwenye kuyaamini mafundisho. Katika hali hii ili mafundisho tuweze kuyaita yetu yanahitajika yawe rahisi na wazi, maadilifu na yakutosheleza katika kuwakilisha mawazo yote yakiwa sahihi kwa maneno yanayotumika katika maisha ya kila siku.

Kitabu hiki ni matokeo ya fikra za hapo juu kikirithi " mkondo" wa Daizokyo yake ya zaidi ya miaka elfu mbili na mamia kadhaa. Ni kweli, kitabu hiki hakichukuliwi kuwa sahihi katika mahudhui yake. Maneno ya Buddha yana maana yenye kina kisicho kikomo na Uadilifu wake hauna kikomo kiasi kwamba mtu hushindwa kuyathamini kwa urahisi.

Kwa hiyo inaaminiwa kwamba kitabu hiki kitazidi kukuzwa na kuzidi kuwa chenye ukweli na thamani kubwa kwa kadri nakala zirudiwavyo na kutolewa siku za usoni, kama ilivyoazimiwa.

## HISTORIA YA "MAFUNDISHO YA BUDDHA"

Kitabu hiki kinafuata chapa ya asili ya Kijapani iliyokusanywa na kupitiwa, iitwayo Newly Translated Buddhist Text kilichochapishwa mnamo Julai, 1925, na Shirika la Kueneza Kitabu cha "Newly Translated Text" lililoongozwa na kasisi Muan Kizu. Chapa hii ya kwanza ya Kijapani ilikusanywa na kuandikwa na Profesa Chizen Akanuma, wakishirikiana na wasomi wengi wa ki - Buddha katika Ujapani na ikachukua karibu miaka mitano kukichapisha.

Katika kipindi cha Showa (1926 - ) kitabu cha Popular Edition of Buddhist Text katika Kijapani pia nacho kilichapishwa na shirika na kuenezwa pote katika Ujapani .

Julai, 1934 wakati wa vijana wa ki-Buddha wa Pan Pacific walipokutana Ujapani, The teaching of Buddha, tafsiri ya kingereza ya Popular Edition of Buddhisttda Text ilichapishwa na Fungamano la vijana wote wa Ki - Buddha katika Ujapani kwa msaada wa Bwana D . Goddard ikiwa ni kama kazi mojawapo ya fungamano hilo. Wakati wa kusherehekea miaka 70 tangu kuanzishwa kwa u - Buddha katika Marekani mwaka 1962, Bwana Yehan Numata, Mwanzilishi wa kampuni ya Mitutoyo, alichapisha toleo la Kiingereza la The Teaching of Buddha yeye binafsi.

Mwaka 1965 wakati Bw. Numata alipoanzisha shirika la kuendeleza u - Buddha katika Tokyo mojawapo ya kazi za shirika hilo zilizopangwa ni kuenezwa kwa toleo la kiingereza dunia nzima.

Ili kutimiza mpango huo kamati ya kupitia The Teaching of Buddha iliundwa mwaka 1966. Wajumbe wa kamati hiyo walikuwa Maprofesa, Kazuyoshi Kino, Shuyu Kanaoka, Zenno Ishigami, Shinko Sayeki, Kodo Matsunami, Shojun Bando, na Takemi Takase. Wengine waliohusika ni Profesa Fumio Masutani, Bw. N.A Wadell, na Bw Toshisuke Shimizu. Kwa hiyo toleo lote la Kiingereza - Kijapani la The Teaching of Buddha lilichapishwa katika mtindo mpya.

Mwaka 1972, Maprofesa Shuyu Kanaoka, Zenno Ishigami, Shoyu Hanayama, Kwansei Tamura, na Takemi Takase walifanya masahihisho ya makosa.

Tena, mnamo 1974 ili kusahihisha misemo isiyo sahihi katika toleo la Kiingereza iliyokuwa imebainishwa na Bw. Richard K. Stainer, kwa shirikisho, chini ya ushauri wake, Maprofesa Shojun Bando, Kodo Matsunami, Shinko Sayeki, Kwansei Tamura, Doyu Tokunaga na Shoyu Hanayama (Mhariri Mkuu) walikipitia kitabu. Katika mwaka 1978 na 1980 kulikuwapo na mkutano juu ya mada zilizopendekezwa na Bw. Shinroku Inouye, wajumbe wa kamati ya uhariri hapo juu pamoja na Profesa Shigeo Kamata na Yasuaki Nara walikutana tena kukipitia kitabu hicho tena. Hivyo basi, toleo la kiingereza-Kijapani la The Teaching of Buddha ilichapishwa katika mtindo wa sasa yakiwa matunda ya kazi yao.

Katika mwaka 1980 ilikubalika kuwa Muda umefika wa kutafsiri kitabu hiki katika lugha zaidi ya nne (Kiingereza, Kifaransa, Kireno na Kihispania) zilizokuwepo. Kwa hiyo, kwa mara nyingine shirika lilimuomba Bw. Steiner kukihakiki kiingereza katika kitabu hicho ili kutafsiriwa katika Kijerumani, Kiitalia, Kigriki, Kichina, Kiholanzi na Kinepali.

Tena, mnamo 1981 ili kukifanya kitabu hiki kiwe rahisi tuliwaomba wanafunzi wa Kijapani na Kimarekani wakisome. Baadaye wahariri walikutana na kuzungumzia mabadiliko pamoja na wanafunzi hawa , na matokeo yake kitabu kilirudiwa na kutolewa upya.

May, 1986

## REJEA YA "MAFUNDISHO YA BUDDHA"


| | Ukurasa | Mstari |
|---|---|---|
| *Maisha ya binadamu* | | |
| Maana ya maisha | 5 | 7 |
| Hali halisi za dunia hii | 90 | 20 |
| Njia adilifu ya maisha | 228 | 17 |
| Maoni potofu juu ya maisha | 42 | 6 |
| Dondoo sahihi la maisha | 39 | 1 |
| Maisha ya mashaka | 54 | 3 |
| Kwa wale waliodanganyika (mfano) | 118 | 14 |
| Maisha ya mtu (mfano) | 85 | 1 |
| Ikiwa mtu ataishi maisha yenye uchafu na tamaa (mfano) | 84 | 6 |
| Yapi yatafundishwa na wazee, wagonjwa na wafu (hadithi) | 87 | 14 |
| Kifo hakiepukiki (hadithi) | 88 | 22 |
| Mambo matano ambayo hakuna ye yote awezaye kuyatimiza duniani | 46 | 2 |
| Kweli nne katika dunia hii | 46 | 11 |
| Madanganyo na Wongofu vyote chimbuko lake ni katika moyo | 47 | 1 |
| Vitu ishirini vya thamani ambavyo ni vigumu mtu wa kawaida kutimiza | 124 | 12 |
| *Imani* | | |
| Imani ni moto | 164 | 6 |
| Imani ina vitu vitatu muhimu | 165 | 15 |

| | Ukurasa | Mstari |
|---|---|---|
| Imani ni matendo | 166 | 17 |
| Imani hujitokeza ndani ya moyo adilifu | 165 | 5 |
| Ni vigumu kutafuta ukweli kama ilivyo vigumu kwa kipofu kujaribu kusimulia sura ya tembo kwa kugusa (mfano) | 70 | 6 |
| Mahali ambapo uasili Buddha upo huonyeshwa kwa mafundisho ya kweli ya u - Buddha (mfano) | 71 | 12 |
| Uasili - Buddha umefichwa na tamaa (mfano) | 72 | 17 |
| Mashaka huzuia imani | 167 | 4 |
| Buddha ni baba wa dunia yote na binadamu ni watoto wake | 33 | 13 |
| Hekima ya Buddha ni pana na yenye kina kirefu kama bahari kuu | 32 | 6 |
| Roho ya Buddha imejaa huruma kuu | 14 | 1 |
| Buddha hana mwili halisi | 15 | 1 |
| Buddha alihubiri katika maisha yake yote | 13 | 1 |
| Buddha alitumia matukio ya maisha na kifo kuwashawishi watu | 21 | 20 |
| Buddha aliokoa watu kutokana na mateso yao kwa kutumia matendo yaliyo kwenye (mfano) | 22 | 2 |
| " | 17 | 13 |
| " | 18 | 11 |
| Dunia ya Uongofu | 230 | 8 |
| Kuwa wafuasi wa Buddha, Dharma na Samgha | 163 | 5 |

| | Ukurasa | Mstari |
|---|---|---|
| Kujifunza njia za kuyatunza maandishi, kujaribu kuutuliza moyo na kutenda kwa uadilifu | 150 | 14 |
| Njia nne takatifu | 153 | 9 |
| Njia sita za kufikia ng'ambo nyingine ya wokovu | 155 | 1 |
| Taratibu nne za haki | 154 | 14 |
| Vigezo vinne vya kufikiria | 154 | 6 |
| Vitivo vitano vya nguvu ya kupatia Wongofu | 154 | 19 |
| Hali nne za moyo zisizo na kikomo | 157 | 5 |
| Wale waelewao hali nne takatifu | 37 | 13 |
| Kifo cha binadamu na maisha ya mpito | 12 | 3 |
| Watazaliwa katika nchi yake takatifu | 106 | 11 |
| Jifanye ni mwanga, jiamini | 10 | 3 |
| *Mafunzo ya akili* | | |
| Yampasa mtu kuyashika yale yaliyo muhimu kwake mwenyewe (mfano) | 139 | 7 |
| Kuwa makini na hatua za mwanzoni | 124 | 8 |
| Usisahau unachokitafuta (mfano) | 140 | 21 |
| Ili kufanikiwa katika jambo lolote yampasa mtu kuvumilia vikwazo vingi (hadithi) | 146 | 6 |
| Jipe moyo hata wakati unapozidi kutofanikiwa (Hadithi) | 158 | 16 |
| Usifanye moyo wako usumbuliwe hata wakati wa hali zisizoridhisha (hadithi) | 115 | 13 |
| Wale waelewao na kufuata njia takatifu ni sawa na kwenda gizani ukiwa na taa | 38 | 5 |

| | Ukurasa | Mstari |
|---|---|---|
| Mtu atakuta mafundisho juu ya maisha ya binadamu popote aendapo (Hadithi) | 149 | 1 |
| Watu huelekea upande waelekezwao na moyo wao | 113 | 13 |
| Maana ya kujifunza ni kumiliki moyo wako mwenyewe | 10 | 19 |
| Umiliki moyo wako kwanza | 194 | 1 |
| Iwapo utamiliki moyo wako | 113 | 17 |
| Hali tofauti za moyo (mfano) | 110 | 10 |
| Moyo si nafsi ya mtu | 44 | 12 |
| Usiruhusu moyo ukuyumbishe | 10 | 6 |
| Uteke moyo wako | 142 | 18 |
| Uwe mtawala wa moyo wako | 11 | 4 |
| Maovu hutoka kwenye mwili, mdomo na moyo | 78 | 18 |
| Uhusiano kati ya moyo na maneno | 117 | 1 |
| Mwili huu si kitu bali jambo la kupotoshwa (Hadithi) | 133 | 8 |
| Mwili huu umejaa kutu za kila aina | 122 | 8 |
| Usitamani chochote | 10 | 6 |
| Takasa mwili, mdomo na moyo | 115 | 10 |
| Usiwe na upendeleo na weka jitihada (hadithi) | 158 | 1 |
| *Mateso ya binadamu* | | |
| Mateso ya binadamu hutokana na moyo wa kufungamana/kupambanua | 41 | 9 |
| Namna ya kuzuia mateso | 12 | 12 |

| | Ukurasa | Mstari |
|---|---|---|
| Madanganyo na ujinga hutengeneza milango ya Uongofu | 56 | 3 |
| Namna ya kujikomboa kutokana na mateso | 108 | 1 |
| Wakati moto mkali wa tamaa unapozimwa, Uongofu wa kustarehesha unaweza kupatikana | 132 | 1 |
| Ngoa ndio hasa chanzo cha madanganyo | 80 | 8 |
| Fikiria ngoa, ufuska kama ni nyoka aliyejificha ndani ya maua | 80 | 9 |
| Usishikamane na nyumba iunguayo (mfano) | 17 | 13 |
| Tamaa ni chanzo cha maovu | 110 | 3 |
| Dunia hii ni moto uunguzao | 77 | 17 |
| Iwapo watu watatafuta umaarufu na heshima, ni sawa na kujiunguza wenyewe | 111 | 8 |
| Mtu akitafuta utajiri na uzinzi, atajiharibu mwenyewe | 111 | 12 |
| Watu wenye busara na wajinga hutofautiana katika asili zao | 125 | 8 |
| Wajinga hawayatambui makosa yao (mfano) | 131 | 12 |
| Ujinga huonea wivu bahati njema ya wengine kwa kuangalia tu matokeo (mfano) | 136 | 15 |
| Njia ambayo wajinga huelekea kufuata (mfano) | 131 | 16 |
| *Maisha ya kila siku* | | |
| Toa sadaka na kusahau | 155 | 21 |
| Aina saba za sadaka bila utajiri | 156 | 4 |
| Namna ya kupata utajiri (Hadithi) | 135 | 9 |
| Jinsi furaha iletwavyo | 123 | 24 |
| Usisahau kamwe wema uliotendewa (hadithi) | 129 | 19 |

| | Ukurasa | Mstari |
|---|---|---|
| Utofauti katika tabia za watu | 83 | 16 |
| Balaa huandamana pamoja na hatua apitiazo mtu atoaye nafasi kwa tamaa ya kulipiza kisasi | 123 | 12 |
| Namna ya kupoza hasira | 225 | 13 |
| Usisumbuliwe na bezo kutoka kwa wengine (hadithi) | 114 | 4 |
| Hamuishi kwa ajili ya mavazi, chakula au malazi | 188 | 7 |
| Chakula na mavazi sio kwa ajili ya raha au starehe | 109 | 1 |
| La kufikiria unapokula | 190 | 15 |
| La kufikiria unapovaa nguo | 189 | 21 |
| La kufikiria wakati unapokwenda kulala | 191 | 6 |
| La kufikiria wakati wa joto au baridi | 190 | 17 |
| La kufikiria katika maisha yako ya kila siku | 189 | 5 |
| *Serikali* | | |
| Njia ya kuelekeza taifa katika fanaka | 210 | 9 |
| Njia kwa mtawala | 213 | 14 |
| Mtawala ajitawale | 211 | 14 |
| Ukweli wa utawala ni kuifunza mioyo ya watu | 212 | 15 |
| Tabia wapaswayo kuwa nayo mawaziri na maofisa | 216 | 13 |
| Namna Jaji apaswavyo kushughulikia wahalifu | 215 | 16 |
| Athari za kuwafunza watu wa taifa | 213 | 8 |
| Namna ya kukabiliana na mapambano ya maisha | 218 | 13 |

| | Ukurasa | Mstari |
|---|---|---|
| *Uchumi* | | |
| Vitu lazima vitumike vizuri (Hadithi) | 202 | 6 |
| Hakuna kitu kilicho mali ya mtu milele | 202 | 1 |
| Mtu asihodhi vitu kwa ajili ya manufaa yake binafsi | 208 | 16 |
| Namna ya kuongeza utajiri (Hadithi) | 135 | 9 |
| *Maisha ya familia* | | |
| Familia ni mahali ambapo mioyo ya wanajamii huunganishwa pamoja | 199 | 17 |
| Vitu ambavyo vitavuruga familia | 194 | 15 |
| Njia za kulipa fadhila mtu atendewazo na wazazi wake | 199 | 10 |
| Njia nzuri za mtoto kufanya kwa wazazi wake | 195 | 14 |
| Njia sahihi za mume na mke | 196 | 14 |
| Mume na mke lazima wawe na imani sawa (Hadithi) | 205 | 1 |
| *Maisha ya wanawake* | | |
| Aina nne za wanawake | 203 | 5 |
| Aina mbali mbali za wake | 205 | 19 |
| Mafundisho kwa wake wachanga (Hadithi) | 204 | 3 |
| Kwa manufaa ya wanawake kuolewa | 204 | 3 |
| Kwa manufaa ya wanawake wachanga na warembo | 207 | 12 |
| Ni vipi wanaume wanaweza kuheshimu wake zao | 121 | 21 |
| Tabia ya wanaume kwa wanawake | 204 | 19 |

| | Ukurasa | Mstari |
|---|---|---|
| Viapo na matakwa ya mwanamke halisi ............... | 208 | 13 |
| Mke mbaya ni yupi? ........................................... | 205 | 19 |
| *Njia ya Ndugu wasio na makazi* | | |
| Mtu hawi ndugu asiye na makazi kwa vile tu anavaa kama mtawa na kutamka maneno matakatifu ya Sutras ........................................... | 180 | 23 |
| Ndugu wasio na makazi sio warithi wa hekalu na vifaa vyake .................................................. | 178 | 1 |
| Watu wenye tamaa hawawezi kuwa watawa wa kweli ......................................................... | 178 | 7 |
| Maisha halisi apasayo kuishi ndugu asiye na makazi (kwao) ............................................ | 179 | 23 |
| *Maisha ya jamii* | | |
| Maana ya maisha ya jamii .................................... | 221 | 8 |
| Hali halisi ya dunia hii .......................................... | 90 | 20 |
| Aina tatu za uongozi ........................................... | 221 | 13 |
| Maisha ya kweli ya jamii ..................................... | 222 | 1 |
| Mwanga mkuu umulikao giza ............................. | 220 | 7 |
| Uelewano katika mahusiano ya watu ................... | 222 | 15 |
| Mambo yatakayosaidia kuiongoza jamii ................ | 223 | 15 |
| Uhalisi wa udugu ............................................... | 222 | 17 |
| Ujamaa halisi wa wafuasi wa u - Buddha .............. | 229 | 22 |
| Wale wavurugao sheria ya amani Wataharibikiwa (mfano) ..................................... | 130 | 19 |
| Wale walio na uvivu na wagombanao na wenzao wataharibikiwa (mfano) ...................................... | 130 | 19 |
| Watunze wazee kwa heshima (Hadithi) ............... | 126 | 1 |

| | Ukurasa | Mstari |
|---|---|---|
| Mwanafunzi apaswavyo kumtendea mwalimu na mwalimu apaswavyo kumtemdea mwanafunzi | 196 | 4 |
| Kanuni za urafiki | 196 | 22 |
| Namna ya kuchagua rafiki wazuri | 198 | 6 |
| Namna ya mtumishi na mtumikiwa wapaswavyo kutendeana | 197 | 7 |
| Namna ya kuwakabili majambazi | 209 | 2 |
| Mambo ya kufikiriwa na wale wanaodhamiria kufundisha Dharma | 182 | 7 |

# REJEA YA SANSKRIT (kufuata mpangilio wa herufi)

**ANĀTMAN (pasipo -nafsi/u-mimi)**

Hii ni mojawapo ya mambo ya msingi katika U - Buddha. Vitu vyote na uhai wote havina maana wala hakika. Ni jambo la kawaida kwa u - Buddha, unaohubiri kutokudumu kwa kila kitu, kusisitiza kuwa kutokudumu kwa vitu vyote hakuwezi tena kuwa na hakika ndani yake. Anātman inaweza kutafsiriwa pia kama isiyo na Roho.

**ANITYA (Hali ya mpito au kutodumu)**

Jambo jingine la msingi katika u - Buddha. Uhai, maisha na vitu, katika ulimwengu huu vinabadilika mara kwa mara bila kukoma angalau kwa kitambo kidogo. Kila kitu lazima kife au kifikie mwisho wake katika siku za usoni mwake, na matazamio haya ndiyo chanzo halisi cha mateso. Dhana hii isitafsiriwe kwa mtizamo wa chuki , au ubaya, kwa sababu uzazi na maendeleo vyote ni udhihirisho wa mabadiliko hayo ya mara kwa mara.

**BODHISATTVA (Anayejitahidi kuipata NURU/ Wongofu)**

Mwanzoni jina hili lilitumika kuonyesha Gautama Siddhārtha kabla hajaipata NURU. Baada ya kutokea u - Buddha wa Mahāyāna wale wote waliojibiidisha na u- Buddha wakajulikana kwa jina hili. Mwisho wale wanaojaribu kuwaelekeza wenzao kwenye udugu wa ki - Buddha kwa njia za huruma kuu huku wakijibiidisha kuelekea kwenye lengo lilelile, wametambulishwa kwa Ishara ya Wabodhisattva; Avalokiteśvara (Kwannon), Kṣitigarbha (Jizō) Mañjuśrī (Mon-ju) ni kati ya wachache wanaojulikana vizuri.

**BUDDHA (Aliyemwongofu)**

Mwanzoni kabisa, Gautama Siddhārtha (Śākyamuni) muasisi wa u - Buddha aliitwa kwa jina hili kwa kuwa ni yeye aliyeipata NURU miaka 2,500 iliyopita, akiwa na umri wa miaka 35 huko India. Shabaha kuu ya wafuasi wa Buddha wote bila kujali mkondo au shule waliomo ni kuwa ma - Buddha. Kwa sababu ya utofauti wa njia za kufikia hali hii, u - Buddha umegawanyika katika madhehebu na shule mbali mbali. Katika u - Buddha wa Mahāyāna mbali na Śākyamuni, Buddha wa kihistoria, Śākyamuni, Mabuddha wengi kama vile Amitābha (Amida),

Mahāvairocana (Dainichi), Vaiṣajyaguru (Yakushi) n.k. wanakubalika kama alama za mafundisho ya u - Buddha. Wakiwa wameathiriwa na dhana ya u - Buddha wa imani ya Nchi Takatifu katika Ujapani (mtu anakuwa m - Buddha baada ya kuzaliwa tena katika Nchi Takatifu) wale wote waliokufa wanaitwa "ma - Buddha," au HOTOKE katika kijapani.

**DHARMA (Mafundisho ya Kweli)**

Haya ni mafundisho aliyofundisha Buddha, Aliyebarikiwa. Kuna aina tatu za kanuni katika mafundisho: Sūtras, (Mafundisho ya Buddha mwenyewe), Vinayas, (maadili yatolewayo na Buddha),na Abhidharmas, (fafanusi na mazungumzo juu ya Sūtras na Vinayas zilizotolewa na wasomi katika vipindi vya baadaye). Kanuni hizi tatu zinaitwa Tripiṭaka. Dharma ni moja kati ya hazina tatu za u - Buddha.

**KARMAN (Matendo)**

Ingawa maana ya asili ya neno hili ni "matendo", katika kuhusiana na nadharia ya chanzo limetokea kutambuliwa kama namna ya uwezo/ nguvu iliyotokana na kila tendo lililotendwa na mtu siku za nyuma. Hii ina maana kuwa kila moja ya matendo yetu hutokea katika wema au ubaya, mateso au furaha ikitegemeana na tendo lenyewe na lina uwezo wa kuathiri maisha yetu ya ahera, na hii inatambuliwa kama Karma ya mtu. Kuna kuamini kuwa tendo jema likirudiwa, wema utajumuishwa na uweza wake na utatenda kazi juu ya maisha ya ahera kama athari yenye manufaa. Kuna aina tatu za matendo; ya mwili, ya kauli na ya akili katika dhana hii.

**MAHĀYĀNA (Gari Kuu)**

Katika uelekeo wa historia ya u - Buddha ilitokea mikondo miwili ya mawazo, Mahāyāna na Theravāda (au Hīnayāna). U - Buddhawa ki - Mahāyāna ulienea Tibeti, Uchina, Korea, Ujapani n.k wakati u - Buddha wa Theravāda ulienea Burma, Śrī Lanka (Ceylon), Thailand n.k. Neno Mahāyāna lamaanisha "Gari kuu" linaloweza kubeba viumbe wote wanaoteseka katika dunia hii ya uzao na kifo, na linaloweza

kuwaongoza wote katika NURU bila kuwabagua.

**NIRVĀṆA (Utulivu Kamili)**

Maana yake ni "Kuungua". Hii ni hali ambapo uchafu wote wa binadamu na mateso vimeteketezwa kabisa kutokana na matendo na tafakuri kwa msingi wa Hekima Sahihi. Wote waliopata hali hii wanaitwa Mabuddha. Gautama Siddhārtha aliipata hali hii katika umri wa miaka 35 na akawa Buddha. Hata hivyo, inaaminika kwa sasa kuwa aliifikia hali ya raha mstarehe kamili baada ya kufa kwake, kwa sababu mabaki ya uchafu wa kibinadamu yangeendelea kuwepo ili mradi mwili wake halisi unaendelea kuishi.

**PĀLI (Lugha)**

Hii ni lugha iliyotumika katika u - Buddha wa Theravāda. Fungu la kanuni za zamani za u - Buddha ziliaminika kwa kuwa ziliandikwa katika Lugha hii. Kwa kuwa hii ni namna ya Praknt, lahaja ya Sanskrit, hakuna tofauti kubwa kati ya Pāli na Sanskrit, Dharma katika Sanskrit. Dharma katika Pāli, Nirvāṇa katika Sanskrit, Nibbāna katika Pāli, (Angalia - Sanskrit).

**PĀRAMITĀ (Kuvuka hadi ng'ambo ya pili)**

"Kuvuka hadi ngambo ya pili" ina maana ya kufikia katika nchi ya Buddha kwa kushika na kutenda maadili mbali mbali ya Buddha. Kwa kawaida maadili sita ya utendaji yafuatayo yanatambuliwa kuwa ni yale yanayomfanya mtu avuke kutoka katika ulimwengu huu wa uzawa na mauti hadi kwenye ulimwengu wa NURU. Sadaka (Matoleo), Uadilifu, uvumilivu, juhudi, umakini na Uamuzi sahihi (au Hekima). Majuma ya HIGAN katika utamaduni wa Kijapani katika majira ya kuchipua na vuli yanatokana na dhana hii ya ki - Buddha.

**PRAJÑĀ (Hekima)**

Ni mojawapo ya Pāramitās sita. Kazi ya akili inayomwezesha mtu kutambua maisha bila kukosea na kutofautisha kati ya ukweli na uwongo. Mtu alipatapo hili kwa usahihi huitwa Buddha. Kwa hiyo hii ni hekima iliyosafishwa na kutakaswa, tofauti na akili za binadamu za

kawaida.

**SAṀGHA (Udugu wa ki - Buddha)**

Ina - maanisha watawa wa kike na kiume, walei wa kike na kiume. Katika siku za kwanza iliwahusu watawa wa kike na kiume wasiokuwa na maskani. Baadaye, wakati mwamko wa Mahāyāna ulipoibuka, wale wote waliolenga kwenye Bodhisattva, bila kujali kama walikuwa walei au watawa, walijiunga pamoja katika undugu. Mojawapo ya hazina tatu za u - Buddha.

**SANSKRIT (Lugha)**

Lugha ya asili, ya kale ya India mojawapo ya lugha zilizotumiwa na familia za kihindi - Ulaya. Imegawanywa kwenye vedic na Sanskrit halisi. Maandishi ya asili ya Mahāyāna yameandikwa kwenye lugha hii katika mtindo ujulikanao kama U-Buddha uliobobea kwa Sanskrit (Buddhist Hybrid Sanskrit)

**SAṀSĀRA (Kurudi katika mwili)**

Marudio ya mara kwa mara ya uzawa na mauti kuanzia zamani, hadi leo na siku zijazo hupitia katika falme sita danganyifu: Jehanam, pepo zenye njaa, wanyama Aśura au Pepo zipiganazo, watu na peponi. Mpaka hapo mtu aipatapo nuru hawezi kukwepa gurudumu hili la kuhama kwa roho. Wale wote walio huru katika hii wanaweza kuitwa ma - Buddha.

**ŚŪNYATĀ (Pasipo - Hakika) (Pasipo - Asili)**

Hii ni dhana kuwa kitu hakina uhakika wa kudumu na ni mojawapo ya mambo ya msingi katika u - Buddha. Kwa kuwa kila kitu kinategemea sababisho haiwezekani kuwepo kwa nafasi ya kudumu kama asili au hakika. Lakini mtu asing'ang'anie kwenye dhana ya kwamba kila kitu kina hakika wala hakina. Kila kiumbe kiwe binadamu au si binadamu, kipo katika uwiano. Kwa hiyo ni ujinga kung'ang'ania wazo moja au dhana fulani au itikadi kana kwamba ndiyo kauli pekee. Haya ni maelekeo ya msingi katika maandiko ya Prajñā ya u - Buddha wa Mahāyāna.

**SŪTRA (Maandiko)**

Kumbukumbu za mafundisho ya Buddha Maana ya awali ni "Uzi," inayomaanisha kufunga maandiko kwa pamoja na kwa ufupi au muhtasari kutokana na mafunzo lukuki ya dini au elimu.

**THERAVĀDA (au Hīnayāna : Watetezi wa Wazee)**

Utamaduni wa kusini wa u - Buddha unawakilishwa na jina hili. "Thera" maana yake wazee. Hii ni shule ya wazee ambapo kihistoria kilikuwa ni kikundi cha watawa wenye kushikilia mambo ya kale na waliopendelea kuyafuata mafundisho kwa makini kinyume na kikundi kingine cha watawa kilichokuwa huru (ambao imani zao baadaye zilidhihirika katika Mahāyāna ndio utamaduni wa Kaskazini). Huu mkondo wa upinzani katika madhehebu ya Ukuhani wa ki - Buddha unasemekana ulianza mapema sana karne chache baada ya kifo cha Buddha, wakati Mahādeva mtawa mwenye mageuzi alipokazania tafsiri huria chini ya makundi matano ya mafundisho ya u - Buddha. Hii ilisababisha mgawanyiko katika Theravāda na Mahāsāṁghika ambapo ilikuwa chemuchemi ya Mahāyāna ya baadaye.

**TRIPIṬAKA (vikapu vitatu)**

Matawi matatu ya maandiko ya u - Buddha, Dharma, yana maana hii. Haya ni Sūtra, yenye mafundisho ya Buddha; Vinayas, yenye maadili yake, na Abhidharmas zenye fafanuzi na habari juu ya imani na mafundisho. Hapo badaye maandishi ya ki - Buddha yaliyoandikwa na makuhani - Wakuu wa kichina na Kijapani yaliingizwa katika kanuni za u - Buddha. Angalia - Dharma.

Watawa, kuna mtu mmoja ambaye uzawa wake katika dunia ni kwa manufaa ya wengi, kwa furaha ya wengi: aliyezaliwa kutokana na huruma kwa ajili ya dunia, kwa faida, manufaa na furaha ya viumbe wa mbinguni na binadamu. Mtu huyo ni nani? Ni Tathagata ambaye ni Arahat, huyu mtawa, ni mtu yule mmoja.

Watawa, ufunuo wa mtu mmoja ni nadra kuupata katika dunia. Wa mtu yupi? Tathagata ambaye ni Arahat, aliyeupata wokovu kamili. Ni yule mtu huyo mmoja.

Watawa vigumu kupatikana duniani ni mtu yule wa ajabu. Mtu yupi? Tathagata ambaye ni Arahat, aliyeupata wokovu kamili. Ni mtu huyo huyo mmoja.

Watawa, kifo  cha mtu mmoja ni lazima kimsikitishe kila mmoja. Cha mtu yupi? Cha Tathagata ambaye ni Arahat, Aliyeupata wokovu kamili. Ni mtu yule mmoja.

Watawa, vigumu kupatikana duniani ni mtu yule wa ajabu. Mtu yupi? Tathagata aliye Arahat, aliyeupata wokovu. Ni mtu huyo mmoja.

Watawa, kuna mtu mmoja azaliwaye duniani ambaye hana ulinganisho wala usawa. Mtu huyo ni nani? Ni Tathagata ambaye ni Arahat, aliyeupata wokovu kamili. Ni mtu huyo mmoja.

Watawa, ufunuo wa mtu mmoja ni ufunuo wa jicho kuu, mwanga mkuu, nuru kuu. Wa mtu yupi? Wa Tathagata ambaye ni Arahat, Aliyepata wokovu kamili. Ni nani huyo mmoja (Aṅguttara Nikāya 1-13).

TAASISI YA KUENDELEZA NA KUENEZA
U-BUDDHA NA USAMBAZAJI WA

## "MAFUNDISHO YA BUDDHA"

Katika kuendeleza u-Buddha ni muhimu kumzungumzia mfanyabiashara, na muungwana huyu ni Bwana Yehan Numata, mwanzilishi wa Kampuni ya uundaji ya Mitutoyo.

Alianzisha Kampuni ya kutengeneza zana za kuonyesha vipimo halisi katika mwaka 1934. Imani yake ni kuwa kufaulu kwa biashara hutegemea uhusiano wa karibu sana wa mbinguni, duniani na binadamu, na kwamba ukamilifu wa moyo wa binadamu unapatikana tu kwa uhusiano unaowiana wa hekima, huruma na ushupavu.

Kutokana na imani hii anafanya kila anachoweza kuendeleza ufundi wa utengenezaji wa zana za kupimia na kuendeleza moyo wa binadamu.

Ni imani yake kuwa kupata amani ya ulimwenguni kunawezekana tu kutokana na ukamilifu wa moyo wa binadamu kwa shabaha yenye mafundisho ya Buddha. Kwa hiyo mbali na kuongoza kampuni yake amekuwa akijibidiisha tangu mwanzo katika kueneza na kuboresha muziki wa kisasa wa ki-Buddha pamoja na kusambaza picha na mafundisho yake.

Desemba, 1965, aliimarisha taasisi kwa fedha zake binafsi katika shughuli za kutangaza u-Buddha na wakati ule ule kutoa msaada kwa ajili ya amani ya dunia. Kwa hiyo taasisi ya kueneza u-Buddha ikaanza kama taasisi ya umma.

Ni nini kinachofanyika katika kueneza mafundisho ya u-Buddha kwa marefu na mapana ili kila mmoja afaidike na kufurahia Mwanga na Hekima yake kuu na Huruma?

Ni kazi ya hii taasisi ya kuendeleza u-Buddha kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili, kwa kuzingatia wosia wa mwanzilishi wake. Kwa kifupi kila juhudi inayofanywa katika kutangaza mafundisho ya Buddha inakidhi haja ya Taasisi ya kuendeleza u-Buddha.

Kitabu hiki "Mafundisho ya Buddha" ni matokeo ya fikra zetu juu ya historia ya dini katika nchi hii, kwamba hapajakuwepo kitu chochote kilichoandikwa na tukakiita kitabu cha Mafundisho ya u-Buddha kama inavyotafsiriwa katika mtizamo wa Kijapani kwa uelekeo wake ingawa tumekuwa tukiheshimu utamaduni wa ki-Buddha kwa fahari kubwa.

Kitabu hiki kitatumika kama "chakula" cha kiroho kwa mtu ye yote atakayekisoma. Kimeandikwa jinsi kilivyo ili mtu ye yote aweze kukiweka katika meza yake au kwenda nacho na kukutana na mwanga wa kiroho kwa utashi wake.

Ingawa hakijafikia ukamilifu kama jinsi ambavyo tungependa, toleo la sasa la "Mafundisho ya Buddha" limetokea mbali, na limetokana na kazi na juhudi za watu wengi kwa nia ya kukidhi mahitaji ya watu wa kisasa kwenye kuanzisha u-Buddha unaokubalika na wenye maandishi yaliyo sahihi ambayo ni rahisi kusomeka na kueleweka, wakati ule ule yakawa ni mwongozo wa matendo na rejea ya kila siku na hamasa ya kweli.

Ni shauku na matumaini ya taasisi ya kueneza u-Buddha kuona siku inafika ambapo nyumba nyingi zinakuwa na kitabu hiki na watu wengi sana wanafurahi na kuoga katika mwanga wa Mwalimu Mkuu.

Maoni ya wasomaji yanakaribishwa.

Tafadhali jisikie huru kuiandikia taasisi ya kueneza na kuedeleza u-Buddha wakati wo wote.